TAARIFA YA MAANDALIZI YA SHEREHE YA KUTANGAZWA MJI MKONGWE WA MIKINDANI KUWA MJI WA KITALII TAREHE 20/02/2017

1.0 UTANGULIZI

Mnamo mwezi Januari 2017,Mkurugenzi wa Manispaa Mtwara-Mikindani alipokea barua toka kwa Mkuu wa Idara ya mambo ya Kale wa Mji wa kihistoria wa Mikindani ikimjulisha maagizo ya barua toka wizara ya Maliasili na Utalii ikimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa kuwaondoa wakazi wanaoishi kwenye Nyumba hatarishi katika Mji mkongwe Mikindani baada ya kupokea taarifa ya majengo yaliyotambuliwa kuwa hatarishi.Mkurugenzi alipokea barua na kuanza utekelezaji wa kuendesha kikao na Wataalam wa Sekta mbalimbali akishirikisha shirika la Trade Aid ambalo ni mdau wa maendeleo eneo la Mikindani,kikao hicho kilifanyika Tarehe 17/03/2017.Kikao hicho kilipendekeza majina ya Watu ambao wataunda Kamati ndogo ya kushughulikia masuala ya Mikindani kwa nia ya maandalizi ya kutangazwa kuwa Mji wa kitalii. Mapendekezo ya majina hayo yalifikishwa kwenye kikao cha kamati kubwa iliyohusisha madiwani wa Tarafa ya Mikindani na Mstahiki Maya tarehe 24/03/2017.Kupitia kikao hicho kamati iridhia mapendekezo ya waliopendekezwa kuwa wajumbe wa Kamati ndogo na kuwapa majukumu ya kushughulikia yafuatayo:-

Kutembelea majengo hatarishi,kufanya makisio ya ukarabati,kuongea na wamiliki/wakazi wa Nyumba hizo,kuainisha majengo ambayo yatapewa kipaumbele kama vivutio vya watalii,maandalizi ya sherehe ya Mikindani kutangazwa kuwa Mji wa Kitalii,kubadili matumizi ya jengo la shule ya zamani ya wajerumani litumike kwa shughuli za kitalii,uondoaji wa mabanda yaliyozunguka Gereza la zamani katika Mji Mkongwe wa Mikindani na kutafuta waalimu wa Lugha mbalimbali za kigeni na kuwafundisha Vijana hasa wa Mikindani na Mtwara Mjini ili wapate nafasi katika shughuli mbalimbali kwa kuweza kuwasiliana na wageni.Wajumbe walitekeza mmagizo ya Kamati kuu kama taarifa hii inavyoelezea kipengele kwa kipengele.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUU

2.1 UKAGUZI WA MAJENGO YA KALE HATARISHI

Kamati ilifanya ukaguzi wa Majengo hatarishi,na jumla ya Majengo 78 yalitambuliwa kuwa katika hali hatarishi kwa maisha ya binadamu

2.2 MAKADIRIO YA GHARAMA

Kamati kupitia Halmashauri na Trade Aid iliwaajiri mafundi wenye ujuzi wa ukarabati wa majengo ya Kale ili kuweza kufanya makadirio ya ukarabati wa majengo hayo,tayari makisio yameandaliwa yanasubiri kupitiwa na Afisa wa mambo ya kale,tayari kwa kuyarasimisha.

2.3 ORODHA YA MAJENGO YA KUPEWA KIPAUMBELE

Kamati baada ya kukagua majengo hatarishi ilipendekeza majengo yafuatayo kupewa kipaumbele;

- Kisima cha asili cha Haikata
- Gereza la zamani
- Nyumba aliyoishi Dr Livingstone
- Msikiti wa Shiha
- Makaburi ya Waingereza na DC
- Soko la watumwa
- Old Boma
- Nyumba aliyolala Mwl Julius .K. Nyerere

2.4 JENGO LILILOTUMIKA KAMA SHULE NA BAADAYE ZAHANATI KUWA HOTEL

Kamati ilitekeleza jukumu la kubadili matumuzi ya jengo lililotumika kama shule enzi ya ukoloni,na baadaye kama Zahanati ili litumike kwa shughuli za kijamii na kitalii kwa sababu lipo karibu na Soko la Vyakula vya asili na baharini kama lilivyo Soko la Forodhani Zanzibar.Baadhi ya wajumbe wa kamati waliwasiliana na Mganga Mkuu wa Manispaa na kujadili suala la jengo hilo na kufikia muafaka litumike katika shughuli za kijamii na kitalii.

2.5 UONDOAJI WA VIBANDA VILIVYOJENGWA NDANI YA ENEO LA GEREZA LA ZAMANI

Kamati kupitia mijadala ya uelimishaji wa umuhimu wa kuondoa vibanda hivyo kwa wamiliki wa vibanda ulifanyika kupitia vikao mbalimbali na hatimaye wenye vibanda walibomoa vibanda vyao ili kupisha zoezi la ukarabati

2.6 KUTAFUTA WAALIMU WA LUGHA MBALIMBALI

Kamati ilitekeleza jukumu hilo kupitia Halmashauri na Trade Aid kwa kutafuta waalimu wa masomo ya kifaransa,kijerumani, kiispania na kijerumani,na tayari waalimu wamepatikana

2.7 MAANDALIZI YA SHEREHE YA MIKINDANI TAREHE 20/02/2018

Kamati ilitekeleza jukumu la maandalizi ya sherehe ya siku ya Mikindani kwa kufanya yafuatayo;

- Halmashauri imeshirikiana na Shirika la Trade Aid kuandaa eneo la bustani kwa kupanda maua,miti na kuweka zulia la ukoka na viti vya asili vilivyotengezwa kwa kutumia mbao kutoka miti ya asili,mfumo wa maji na umeme umewekwa na tayari biashara ya kahawa na supu ya pweza vimeanza kuuzwa
- Vikundi vya Wanawake 2 na Vijana 1 vimeandaliwa na kupata mafunzo ya jinsi ya kuendesha biashara kupitia Trade Aid ili kutumia fursa ya kufanya biashara ya vyakula vya asili na baharini kupitia upishi wa njia za asili na Manispaa itawapa mkopo ili viweze kununua vitendea kazi kama majiko,vyombo na mtaji wa kununa chakula.

3.0 KUTANGAZWA MJI MKONGWE WA MIKINDANI KUWA MJI WA KITALII

Kupitia Tangazo la Serikali namba **308** la tarehe **25/08/2017**, Mji mkongwe wa Mikindani umetangazwa kuwa mji wa kitalii na baada ya kutangazwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliiomba Halmashauri ya Manispaa Mtwara Mikindani ishirikiane na shirika la Trade Aid Tanzania kufanya maandalizi ya maadhimisho ya kusherekea uamuzi huo nzuri uliofanywa na Serikali na mapendekezo ya maandalizi hayo yafikishwe ofisini kwake.

Agizo hilo lilitekelezwa na Mkurugenzi kwa kuitisha kikao cha Kilichoshirikisha kamati ndogo inayoshughulikia masuala ya Mji Mkongwe wa Mikindani kuanzia mwezi Machi 2017. Kikao kilifanyika tarehe 28/11/2017 na kukubaliana yafuatayo;

3.1. MGENI RASMI NA WAGENI WAALIKWA NGAZI YA KITAIFA NA KIMATAIFA

Kamati ya maandalizi imewasiliana na ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa lengo la kumuomba kuridhia mapendekezo ya kumwalika makamu wa Rais au Waziri Mkuu kuwa mgeni rasmi,pia mabalozi wa Nchi zifuatazo;

- Uingereza
- Ujerumani
- Marekani,
- Sweden
- Seychelles.

Katibu tawala Mkoa aliiagiza kamati kuandaa barua za mialiko na kuzifikisha ofisini kwake na kupanga kikao kitakachomshirikisha Katibu Tawala Msaidizi,wawakilishi wa Kamati na Katibu Tawala Mkoa ili kuweza kukubaliana.Kikao kilichomshirikisha Katibu Tawala kilifanyika tarehe 18/12/2017,

na kupitia kikao hicho Katibu Tawala aliridhia mapendekezo ya Kamati na kuwaomba kuendelea na maandalizi.

3.1.2 ENEO LA SOKO LA VYAKULA

Kikao cha kwanza cha kamati kuu kilichofanyika tarehe 17/03/2017 kwa lengo la kutekeleza agizo la Wizara ya maliasili na utalii katika maandalizi ya Mikindani kutangazwa kuwa Mji wa Hifadhi ya Mambo ya Kale ,kilianisha eneo la kutengenezwa bustani litakalotumika kama soko la vyakula vya asili na baharini kama ilivyo forodhani Zanzibar na kuipa Kamati ndogo jukumu la kuendeleza eneo hilo kuwa bustani.Tayari eneo limeendelezwa kwa kutengeneza bustani ya maua na zulia la ukoka,maji na umeme vimewekwa na choo kipo katika hatua za mwisho kukamilika.

3.1.3 MAENEO YATAKAYOFUNGULIWA SIKU YA SHEREHE

Kamati ya maandalizi imependekeza maeneo/vitu vifuatavyo vifunguliwe siku ya sherehe,

- Kisima cha asili cha Haikata-Hiki ni kisima ambacho chimbuko lake ni waarabu ,walikichimba kwa ajili ya kilimo cha Minazi na Miembe mnamo karne ya15.Ulipofika utawala wa wajerumani waliamua kuboresha kwa kukijenga ili kuimarisha Mwaka 1895,na utawala wa Waingereza walikikarabati Mwaka 1946 na Mwaka 2017 Trade Aid imekikarabati.Kisima hiki kilitumiwa na wakoloni na Wananchi wa Mikindani,ni kisima cha asili kisichokauka maji
- Ujenzi wa uzio wa Gereza la zamani-Gereza lilijengwa na Mwarabu kwa ajili ya biashara ya utumwa,lilitumika kutunza watumwa.Ulipoingia utawala wa Wajerumani liliendelea kuwa gereza lakini lilitumika kufunga waalifu,eneo linguine chumba cha biashara na kutoza ushuru,kituo cha Polisi,na utawala wa Mwingeza uliendeleza gereza la waalifu,kituo cha Posta na simu,pia kulikuwa na Nyumba ya Gavana wa kiingereza.Mwaka 1914 katika viata kuu ya kwanza ya Dunia jengo liliharibiwa kwa kupigwa bomu na Mwingireza.
- Soko la chimbuli la vyakul (kama forodhani Zanzibar)
- Ufunguzi wa makumbusho ya jengo la Dr. Livingstone-Historia ya jengo inaanzia Mwaka 1866 kupitia DR. Livingstone ambaye aliweka kambi kwa kufunga hema na kuishi katika eneo ambalo limejengwa Nyumba inayotumika kama kumbukumbu yake katika safari yake ya kueneza neno la Mungu,kufanya utafiti wa Mto Nile na kupinga biashara ya utumwa.Katika eneo hilo kiliwekwa kibao cha Dr Livingstone kama kumbukumbu.Mnamo Mwaka 1950 Raia mmoja wa kihindi aliomba idhini ya kujenga Nyumba katika eneo hilo ili kuhifadhi kumbukumbu za safari ya Dr.Livingistone.

3.1.4 MAENEO YATAKAYOTEMBELEWA NA WAGENI

Kamati imependekeza maeneo yafuatayo yatembelewe na wageni;

- Jengo la Old Boma km 1 toka standi ya Mikindani
- Soko la watumwa Km 0.3 toka kituo cha basi Mikindani
- Benki ya zamani km 0.3 toka standi ya Mikindani
- Nyumba ya Dr Livingstone km 0.3 toka standi ya Mikindani
- Msikiti wa zamani wa Shia Km 0.5 toka standi ya Mikindani
- Gereza na ofisi ya Ushuru ya Wajerumani na waingereza Km 1 toka standi ya Mikindani
- Makaburi ya Waingereza na DC wa kwanza Km 2 toka standi ya Mikindani
- Nyumba aliyotumia Mwalimu Julius.K. Nyerere mwaka 1953 wakati wa kupigania Uhuru Km 0.5 toka Standi ya Mikindani
- Kisima cha asili cha HaikataKm 1.6 toka standi ya Mikindani

3.1.5 MAAFALI YA VIJANA WA MIKINDANI WANAOMALIZA MAFUNZO YA HOTELI

Kutafanyika maafali ya Vijana 19, wakiwemo wanaume 5 na Wanawake 14 wa Mikindani watakabidhiwa vyeti vya kufuzu Mafunzo ya hotel yanayotolewa na Trade Aid Tanzania.

4.0 HITIMISHO

Taarifa hii inaletwa kwenye kikao cha DCC ili wajumbe wafahamu hali ya Mikindani kwa sasa kupitia kutangazwa kuwa mji wa hifadhi ya historia ya mambo ya kale .

Aidha muonekano wa majengo hautakiwi kubadilishwa,ata kama yanakarabatiwa, yanatakiwa kutopoteza uhasilia wake.Wajumbe wa DCC wanatakiwa kuelimisha Wananchi wa Mikindani na Manispaa kwa ujumla kuhusu Mji wa kitalii na masharti yake.